




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 29: Msimu wa Kilimo 2020/2021 Tathmini ya Julai 1-10, 2021 na Matazamio Kipindi cha Julai 11-20, 2021

MUHTASARI


- Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa zinaweza kuathiri mazao yaliyohifadhiwa vibaya.
- Hali ya ukavu ikiambatana na upepo mkali inaweza kuathiri upatikanaji wa maji kwa ajili yashughuli za umwagiliaji.
- Upepo mkali unaotarajiwa hususan katika maeneo ya pwani unaweza kuathiri shughuli za uvuvi
- Wafugaji wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kufuata ushauri wa maafisa ugani.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2021

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyoko kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii iliendelea kuushikilia mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi na hivyo kuongeza mwendo kasi wa upepo hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi. Joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la pembe ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa na mchango katika kusukuma hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo ya nchi. Joto la juu ya wastani upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilipunguza kasi ya upepo uvumao kutoka magharibi mwa misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi. Kwa ujumla, mifumo ya hali ya hewa tajwa hapo juu, ilisababisha maeneo mengi ya nchi kuendelea kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi ikiambatana na upepo.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2021

Kwa ujumla, maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu na yenye ubaridi isipokua maeneo machache katika mikoa ya Arusha, Mara, Mwanza, Kilimanjaro, visiwa vya Unguja and Pemba, Rukwa, na Mbeya ambayo yamepata mvua za nje ya msimu kati ya mm 26 na 50 kama inavyoonekana katika kielelezo.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa kipindi cha Julai 1-10, 2021

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2021

Hali ya ukavu iliyojitokeza katika maeneo mengi ya nchi ilisaidia katika shughuli za uvunaji, ukaushaji na utunzaji wa mazao. Kwa maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hakuna shughuli za kilimo zilizoripotiwa isipokuwa maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi hususan mkoa wa Mbeya, Iringa, Kigoma na Dodoma ambapo wakulima walikuwa wanaendelea na uvunaji wa mahindi. Zao la mpunga lipo katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi, Iringa, Mwanza, Shinyanga, Morogoro na Tabora ambapo baadhi ya wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji. Kwa ujumla, hali

ya mazao na mavuno katika maeneo hayo ni ya kuridhisha. Maji na malisho ya mifugo vilikuwa katika hali ya kuridhisha isipokuwa katika mikoa ya Dodoma na Tabora ambako kumeripotiwa upungufu wa maji.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2021

Katika dikadi hii, kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kupungua kutokana na vipindi vya ukavu.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2021

Katika kipindi hiki cha dikadi, migandamizo mikubwa iliyopo kusini inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuushikilia ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi na hivyo kuongeza mwendo kasi wa upepo hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi. Wakati huo huo, upepo wenye ubaridi inatarajiwa kuendelea kusukumwa kutokea kizio cha kusini kuelekea katika maeneo mengi ya nchi. Hali hii inachagizwa na matarajio ya uwepeo wa joto la bahari la chini ya wastani maeneo ya pembe ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Joto la bahari la juu ya wastani upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kupunguza kasi ya upepo uvumao kutoka magharibi mwa misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Kwa ujumla, mifumo tajwa ya hali ya hewa, inatarajiwa kusababisha maeneo mengi ya nchi kuendelea kuwa makavu na yenye hali ya ubaridi.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2021

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata vipindi vifupi vya ngurumo za radi katika maeneo machache. Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kupata hali ya ukavu na baridi kwa ujumla nyakati za usiku na alfajiri na vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo ya miinuko. Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)

yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache yakiambatana na hali ya ubaridi. Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mikoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2021

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi itasaidia katika shughuli za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao. Hali hii itaathiri upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi vinavyotarajiwa katika maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani vinaweza kuathiri ukaushaji wa mazao na shughuli za uvunaji. Hali ya baridi inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi inaweza kuathiri uzalishaji wa mifugo na ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kutunza chakula cha ziada ili kuepuka upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza siku zijazo. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuata ushauri kutoka kwa wataalamu wa sekta husika. Pia inashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku tano na tahadhari kadri zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2021

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Hata hivyo wananchi na mamlaka husika wanashauriwa kutumia rasilimali maji kwa uangalifu.